**MAHUDHURIO YA KIJIJI KATIKA MKUTANO WA TAREHE 13/12/2022 KWAAJILI YA KUJADILI MUENDELEZO WA MKATA WA KUCHIMBA KOKOTO KATI YA KIJIJI KIHANGAIKO NA MWEKEZAJI CHINA GOLD DEVELOPMENT COMPANY**

| JINA | SAHIHI | JINA | SAHIHI |
|---|---|---|---|
| SAUDA ALLY | S.A | MAULIDI SHABANI | Shabani |
| MWANAIDI RAMADHANI | M.R | Ismaili Pengo | I.P |
| Rehema Ally Kisulu | R.A.K | Masudi Hussen | M.H |
| FATINA SAIDI | F.S | Salumu Saidi | S.S |
| Zawadi Juma | Z.J | Rashidi Alulu | R.A |
| Mwajuma Omari | M.O | Hamisi Juma | Juma |
| Hadija Sulemani | H.S | Tabu Dege | T.D |
| Husna Chuma | H.C | Asha Kisulo | Kisulo |
| Ramadhani Abdala | Ramf | MARIAM BAKARI | M.B. |
| Juma Abdalla | Abdl | MARIAMU RAMADHANI | M.R |
| Rajabu kulambea | Kulam | mwanaheri Ally | M.A |
| Shabani Ally | S.A | Fatuma Jauta | F.J |
| Abuu Rashidi | A.R | Zainabu Idirisa | Z.I |
| Juma Mahundu | J.M | Mwanaheri Juma | M.J |
| Magdalena Rugia | M.R | TABU RAJABU | T.B |
| Tumaini Nyange | T.N | SOKO DEGE | S.D |
| Rajabu Saidi | R.S | Kulwa Idrisa | K.I |
| Juma M. Juma | JMJ | Ally Bakari | A.B |
| Thabiti Shabai | T.S | Pili Rashidi | P.R |

Scanned with CamScanner

| JINA | SAHIHI |
|---|---|
| SALIA RASHIDI | S R |
| Mariam MUSA | M.M |
| HADIJA JAFARI | Jafari |
| SURE SHABANI | S.S |
| Zuhura Ramadhani | Z.R |
| MBEZA KUTUPA | M.K |
| MBARAKA RAMADHANI | M.R |
| WAZIRI MIKAMBA | Mikamba |
| RASHIDA BAKARI | Bakari |
| Mwajuma Ally | M.A |
| MWAJABU KOLI | M.K |
| STEPHANO KANJE | S.K |
| Sabina Emanuel | S. E |
| Elizabet Maleko | Maleko |
| Lungo Ally | L.A |
| MAGRET Rafaeli | M.R |
| JUMA SAIDI | J.S |
| Radhea Ramadhani | R.R |
| Juma Saudi | Saidi |

| | |
|---|---|
| | |

Scanned with CamScanner

**MKUTANO MKUU WA KIJIJI KIHANGAIKO KUJADILI MUENDELEZO NA KUPITISHA MKATABA WA KUCHIMBA KOKOTO KATI YA KIJIJI NA MWEKEZAJI CHINA GOLD DEVELOPMENT GROUP COMPANY LTD**

**AGENDA ZA MKUTANO**

**i)M/kiti kufungua mkutano**

**ii)kujitambulisha**

**iii)kujadili ombi la mwekezaji la kuendeleza mkataba wa kuchimba kokoto katika kijiji cha kihangaiko**

**iv)M/kiti kufunga mkutano**

**AGENDA YA KWANZA: M/kiti kufungua mkutano**

**-Mwenyekiti alifungua mkutano saa 4:25 asubuhi, kama ilivyoada mw/kiti aliwasalimia wananchi na kuwasihi kuwa watulivu muda wote wa mkutano ili waweze kumjadili mwekezaji huyo kwa umakini na kupata maridhiano yaliyo sahihi. Mwisho mw/kiti alitamka kuwa mkutano umefunguliwa.**

**AGENDA YA PILI: KUJITAMBULISHA**

Afisa mtendaji wa kijiji alimtambulisha mwekezaji kwa wananchi na kumpa nafasi ya kuwasalimia. Mwekezaji alisimama nakuwasalimu wananchi, hivyo alijitambulisha jina lake anaitwa ndugu Haijun Li ni mkurugenzi wa kampuni ya China Gold Development Group ltd na yupo hapa kwa niaba ya kampuni , wananchi walimpokea.

**AGENDA YA TATU: KUJADILI OMBI LA MWEKEZAJI LA KUENDELEZA MKATABA WAKE WA KUCHIMBA KOKOTO**

Katika ajenda hii , kwanza Afisa mtendaji aliwasomea wananchi barua ya mwekezaji China Gold Development Group. Katika barua hiyo mwekezaji amomba kundeleza mkataba wake wa kuchimba kokoto kwenye eneo la kijiji lenye ukubwa heka 75'

**MAJADILIANO:**

kwanza wananchi walitaka kufahamu maendeleo ya makubaliano yaliyopita baina ya mwekezaji na kijiji ambapo makubalino hayo yalikuwa ni

- mwekezaji kujenga vyumba vya madara mawili katika shule ya msingi Madesa na kihangaiko na nyumba za walimu katika shule hizo za msingi.

- ajira kwa wananchi wa kihangaiko hasa vijana

Scanned with CamScanner

-bila kusahau makubaliano ya kulipa ushuru wa shilingi elfu mbili kwa kila mzigo wa kokoto unaonunuliwa.

Afisa mtendaji alitoa nafasi kwa mwekezaji kuelezea wananchi mambo ambayo kampuni yake imeyafanya katika kijiji, mwekezaji alisimama na kutoa taarifa ya mambo ya mendeleo waliyofanyia kijiji kama ifuatavyo,

**TATHIMINI YA MAMBO YA MAENDELEO YALIYOFANYWA NA MWEKEZAJI KATIKA MKATABA UNAOISHA:**

-mwekezaji ameweza kujenga vyumba viwili vya madarasa katikanshule ya msingi kihangaiko vyenye thamani ya shillingi million kumi na nane (18,000,000)

- mwekezaji amejenga nyumba ya walimu katika shule ya kihangaiko na kushiriki katika ujenzi wa nyumba za walimu Madesa ambapo vyote kwa pamoja imegharimu shillingi millioni ishirini na mbili na laki tano (22,500,000)

-mwekezaji kuanzia mwaka 2017 mpaka 2022 ameshalipa millioni thelasini na sita kama ushuru katika serikali ya kijiji.

-mwekezaji ameweza kutoa ajira kwa vijana katika mradi huu pia ameweza kutoa mafunzo ya kutumia mashine na ulipuaji wa mawe kwa vijana watano

-pia mwekezaji amekuwa akishiriki katika shughuli za kimaendeleo kwa kutoa kokoto na mawe ili kuweza kufanikisha miradi mbalimbali ya kijiji zahanati , ujenzi wa kituo cha polisi na mambo kama hayo.

Baada ya taarifa hiyo mw/kiti alitoa ruhusa kwa kutano kujali , Afisa mtendaji

alisimama na kuuliza wananchi kama kuna mtu yeyote mwenye hoja au swali kwa mwekezaji, ambapo mjumbe mzee Ramadhani Cheya alisimama na kuuliza , kwa kuwa mwekezaji hakutimiza ahadi zote kwa ukamilifu kama alivohaidi mwanzo je sasa hivi tukimpa mkataba mpya tutakuwa na uhakika gani wa yeye kutimiza na nini kifanyike ikiwa hatotimiza?wanachi walopiga makofi kwa swali hilo na Afisa mtendaji alimkaribisha mwekezaji kwaajili ya kujielezea. Mwekezaji alisimama na kusema kuwa changamoto za kibiashara zilichangia sana wao kushindwa kukamilisha maadhimio yote waliyokubalina na hasa ukizingatia ndio walikuwa waanza biashara lakini akahaidi kukamilisha ahadi zota kwa ukamilifu akipewa muda zaidi.

Mjumbe mwingine Bi Fatuma Ramadhani alitoa hoja ya kuwa mwekezaji apewe muda maalum wa kukamilisha maadhimio yote yatakayopitishwa na kama atashindwa kutekeleza basi atakuwa amevunja mkataba na kijiji, pia mwekezaji ajenge madara mengi zaidi kwani wanafuzi wanakaa chini na kusoma kwa shida. Wananchi walipiga makofi kuashiria kukubaliana na hoja ya mjumbe huyo.

Scanned with CamScanner

Mw/kiti alisimama na kumtaka Afisa mtendaji asome maadhimio mapya yaliyoafikiwa kati ya kijiji na mwekezaji

**MAADHIMIO MAPYA KATI YA KIJIJI CHA KIHANGAIKO NA MWEKEZAJI CHINA GOLD DEVELOPMENT GROUP LTD**

1. Mwekezaji anatakiwa kujenga madarasa mapya matatu katika shule ya Kihangaiko yenye thamani ya shilimgi millioni ishirini na saba (27,000,000)
2. Mwekezaji anatakiwa kujenga madarasa mawili katika shule ya Madesa yenye thamni ya shilingi millioni kumi na nane (18,000,000)
3. mwekezaji anatakiwa kuchangia ujenzi wa nyumba za walimu kwa kutoa mchango wa kototo wakati wa ujenzi wenye thamani ya shillingi milliomi ishirini (20,000,000)
4. Mwekezaji anatakiwa kuongeza ajira kwa wenyeji
5. Kijiji kimepa mwekezaji muda wa miaka miwili ya kutekeleza ujezi wa madarasa
6. kijiji kimemuongezea mwekeaji mkataba wa miaka kumi kwenye eneo la heka sabini na tato (75)
7. kijiji kukutana na mwekezaji kila baada ya mwaka kwaajili ya kupanga miradi ya maendeleo ambayo kijiji inataka mwekezaji aifanye.

Baada ya Afisa mtendaji kusoma maadhimio hayo aliuliza kama wanachi wote wamekubalina na maadhimio na wote walipiga makofi kuonesha kuwa wamekubaliana, pia Afisa mtendaji alimuuliza mwekezaji kama anakubaliana na maadhimio ambapo pia na yeye alikubali.

***AGENDA YA NNE: MW/KITI KUFUNGA MKUTANO***

*Mw/kiti alisimama* na kuwashukuru wananchi wote kwa kufika na kutoa hoja zao pamoja na changamoto zenye kuleta tija katika mamendeleo ya kijiji pia aliwaahidi kusimamia kwa uaminifu maadhimio yote yaliyopitishwa. Mwisho mw/kiti alitangaza mkutano umefungwa.

Bakashanu

Consolatha Bakashana

MTENDAJI WA KIJIJI
KIJIJI CHA KIHANGAIKO
BAGAGMOYO

Martin

Martin Joho

MWENYEKITI WA KIJIJI
KIJIJI CHA KIHANGAIKO
BAGAGMOYO

Scanned with CamScanner